


*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# UZAO WA MWANAMKE NA UZAO WA NYOKA

Leo tutajifunza **UNABII** uliozungumzwa na Mungu **moja kwa moja katika bustani ya Edeni**, mwanzoni kabisa mwa historia ya mwanadamu! Ndiyo! Hii ilitokea mara tu baada ya **Mama Hawa kudanganywa** na kuanguka katika **dhambi** na **kutotii** amri ya Mungu kwa ushawishi wa nyoka, na Adamu **akaamua** *(1 Timotheo 2:14)* kufuata mfano na nyayo za Hawa!

Ndiyo! Hebu sasa tuone andiko kama tunavyosoma katika: **Mwanzo 3:15** *"Nami nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino."*

Je! Huu **uzao wa namna mbili** ni nini? Na maana ya **unabii huu** ni ipi? Ili kupata jibu, hebu turudi nyuma mistari michache kisha tusome: **Mwanzo 3:9–14**

*"Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, U wapi wewe? Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa, kwa sababu nalikuwa uchi; nikajificha. Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula matunda ya mti nilokuagiza usile? Adamu akasema, Hawa uliyenipa awe pamoja nami, ndiye aliyenipa matunda ya ule mti, nikala. Bwana Mungu akamwambia mwanamke, Ni jambo gani hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala. Bwana Mungu akamwambia nyoka, Kwa kuwa umefanya jambo hili, Umelaaniwa kuliko wanyama wote, na*

*kuliko kila mnyama wa mwituni; kwa tumbo utakwenda, Na mavumbi utakula, siku zote za maisha yako;*"

Ndiyo!
Hapa ndipo tunapata **msingi wa unabii huu.**

**"Uzao wako"** katika mstari wa 15 unamrejelea **uzao wa nyoka**, yaani **Shetani**. Neno **"uzao"** linamaanisha **watoto au kizazi**. Sasa je, **watoto wa nyoka** ni akina nani? Na **watoto wa mwanamke** ni akina nani? Unabii huu umeandikwa kwa **lugha ya ishara**, ukizungumza juu ya **MWOKOZI** ambaye: *"ataponda kichwa cha nyoka"*

Kwa maneno mengine, **atamwangamiza kabisa**, kwa kuwa nyoka **huawa kwa kupigwa kichwani**, na si mwilini!

**"Nyoka"** hapa bila shaka anamwakilisha **mdanganyifu mkuu – Shetani!!** *(Rejea na soma 2 Wakorintho 11:3 – "kama vile nyoka alimdanganya Hawa kwa hila yake...")* **Sasa, ni nani huyu atakayekuwa "uzao wa mwanamke"?** Hapo mwanzoni, **Mama Hawa alidhani** kwamba **mwanawe wa kwanza Kaini** ndiye yule "uzao" kama tunavyosoma katika:

**Mwanzo 4:1** "*Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akachukua mimba, akazaa Kaini, akasema, Nimepata mwana kwa Bwana.*"

Lakini wazo hilo **lilipata mwisho mchungu** alipomwona **Kaini akimuua Abeli!** Ndipo wakati mwingi ukapita baada ya hapo, katika **Dunia ya Kwanza**, na **hakuna mengi yaliyoonyeshwa** zaidi ya hayo. Kisha, katika **Dunia ya Pili**, Mungu alimwita **Abramu**, ambaye **"aliabudu miungu mingine"** *(Yoshua 24:2)* kutoka katika **nchi ya Uru**, na akampa ahadi kama tunavyosoma katika:

**Mwanzo 12:1–3** "*Bwana akamwambia Abramu, Ondoka katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya kuwa taifa kubwa, nitakubariki, na*

*kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.*"

Ndiyo! Hapa kuna **AHADI KUU** aliyowekewa Abramu ambaye baadaye akawa **"Ibrahimu"**. Mungu aliahidi kwamba **kutokana na uzao wa Ibrahimu**: *"atakuwepo taifa kubwa, na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."* Lakini ili haya yote yatimie, Ibrahimu alihitaji **mtoto – mrithi!**

Hapo awali, Abramu (jina lake kabla ya kuitwa Ibrahimu), baada ya **kungoja kwa miaka mingi bila kupata mtoto**, alidhani kuwa kutokuwa kwake na mtoto kulimaanisha kuwa:

**MRITHI WAKE** na wa ahadi ile angekuwa **mtumishi wake mkuu**, kama tunavyosoma katika: **Mwanzo 15:2–3** "*Abramu akasema, Ee Bwana MUNGU, utanipa nini, maana mimi ninaenda zangu hali sina mtoto; naye atakayemiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri wa Dameski? Abramu akaongeza kusema, Angalia, hujanipa uzao, na tazama, mtu aliyezaliwa katika nyumba yangu ndiye mrithi wangu.*"

Lakini Mungu **alimwondolea shaka**, kama tunavyosoma:

**Mwanzo 15:4** "*Tazama, huyu hatakuwa mrithi wako; bali atakayekutoka viunoni mwako, huyo ndiye atakayekuwa mrithi wako.*"

Ndiyo! Aliambiwa waziwazi kwamba **MRITHI WA AHADI** angekuwa **mwana atakayezaliwa kutoka kwake mwenyewe!** Lakini baada ya **kuendelea kungoja kwa miaka mingi zaidi**, mkewe Sarai alitambua kuwa **hawezi kumzalia Abramu mtoto**, na hivyo **akamshauri** kama tunavyosoma katika:

**Mwanzo 16:2–4** "*Sarai akamwambia Abramu, Angalia sasa, Bwana amenizuia nisizae; ingia kwa kijakazi wangu; labda nitaweza kupata mtoto kwa njia yake. Abramu akasikiza sauti ya Sarai. Basi Sarai mkewe Abramu akamtwaa Hajiri, yule Mmisri, kijakazi wake, baada ya Abramu kukaa katika*

*nchi ya Kanaani miaka kumi, akampa Abramu mumewe awe mkewe. Akaingia kwa Hajiri, naye akachukua mimba..."*

Ndiyo! Kutoka kwa **Hajiri** — kijakazi wa Sarai, **alizaliwa mtoto wa Abramu!!** Aliitwa **Ishmaeli**, na Abramu alidhani kwamba hatimaye **mrithi wa ahadi** alikuwa **amezaliwa.** Wakati huo Abramu alikuwa na **miaka 86** *(Mwanzo 16:15–16)* Kisha, siku moja mkewe Sarai alipofikia **miaka 90**, na Ibrahimu akiwa na **miaka 99**, tunasoma kilichotokea kama kilivyoandikwa katika:

**Mwanzo 17:16–17** "*Nami nitambariki, tena nitakupa mtoto pia kwa yeye; naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa; wafalme wa watu watatoka kwake. Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi, akacheka, akasema moyoni mwake, Je! mtoto atazaliwa kwake aliye na umri wa miaka mia? Na Sara, aliye na umri wa miaka tisini, atazaa kweli?*"

Ndiyo! **Mungu akamtembelea ibrahimu na ujumbe!** Hapa ndipo **hakikisho la Mungu kwa Ibrahimu** lilipotolewa kwamba hata kwa umri huo, **wangepata mtoto kupitia mkewe Sara!** Hili lilimletea **kicheko na kutokuamini** Ibrahimu!

**Alidhani ni utani!** Hasa kwa kuwa Sara akiwa na miaka 90 tayari alikuwa **ameacha kupata hedhi**, kama tunavyosoma katika: **Mwanzo 18:11** "*Basi Ibrahimu na Sara walikuwa wazee, wenye umri mwingi; na imekoma kwake Sara kuwa na desturi ya wanawake.*"

Ndiyo! Ibrahimu akifikiri yote hayo ni **utani mkubwa wa Bwana**, na akijua kuwa ilikuwa **haiwezekani kimwili** kwa Sara kuzaa watoto, akawa na tumaini kwamba **Ishmaeli ndiye angekuwa mrithi**, kama tunavyosoma katika: **Mwanzo 17:18**"*Ibrahimu akamwambia Mungu, Laiti Ishmaeli angeishi mbele zako!*"

Lakini Bwana alimjibu **kwa uwazi** katika: **Mwanzo 17:19** "*Lakini Mungu akasema, Hakika Sara mkeo atakuzalia mwana; nawe utamwita jina*

*lake Isaka; nami nitaifanya agano langu pamoja naye kuwa agano la milele, na uzao wake baada yake."*

Ndiyo! Yote hayo yalionekana **yasiaminike kabisa kwa Ibrahimu!!**

Lakini kadri miezi ilivyopita... na alipoona **ajabu ya ujauzito wa Sara**, yale yote yaliyokuwa **hayaaminiki**, yakaanza: **Kuaminika!**Na kwa **kuzaliwa kwa Isaka**, **imani ya Ibrahimu kwa Mungu** ilianza kukua na kuimarika zaidi na zaidi, hadi siku moja, Bwana akaamua **kumjaribu!**
Sasa tusome kutoka: **Mwanzo 22:1–2** *"Ikawa baada ya mambo hayo, Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ibrahimu! Akasema, Mimi hapa. Akasema, Umchukue sasa mwanao, mwana wako wa pekee, ambaye wampenda, yaani, Isaka, ukaende katika nchi ya Moria; ukamtoe huko awe sadaka ya kuteketezwa juu ya moja ya milima nitakayokuonyesha."* Sasa maneno haya — *"baada ya mambo hayo"* — yanarejelea mambo yaliyotokea katika sura ya 21:

- **Kuzaliwa kwa Isaka**,
- **Sherehe maalum**,
- **Kumwachisha kunyonya**,
- Na mambo yaliyotokea katika sherehe hiyo kama tunavyosoma katika:

**Mwanzo 21:8–12** *"Mtoto akakua, akachishwa ziwa; Ibrahimu akafanya karamu kubwa siku ya kumwachisha Isaka ziwa. Sara akamwona mwana wa Hajiri Mmisri, aliyemzalia Ibrahimu, akicheka. Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu pamoja na mwanawe; maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. Neno hilo lilimchukiza sana Ibrahimu, kwa ajili ya mwanawe. Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisikuchukize kwa ajili ya huyo mtoto, wala kwa ajili ya mjakazi wako; katika*

*yote Sara aliyokuambia, sikiliza sauti yake; kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa."*

Ndiyo! **Ishmaeli alianza kumdhihaki Isaka**, na Sara alipoona hilo **alihuzunishwa sana**, akamwambia Ibrahimu **awafukuze mvulana huyo na mama yake kutoka nyumbani.** Hili lilimhuzunisha sana Ibrahimu kwa kuwa: **Ishmaeli pia alikuwa mwanawe!** Lakini Mungu alimwambia Ibrahimu **kufanya kama Sara alivyosema**, na akaamuru — Na mapema asubuhi iliyofuata **akawapeleka HAGARI na ISHMAELI** pamoja na mkate na maji.

Hivyo basi, **aliyebaki nyumbani alikuwa Isaka peke yake**, na kwa kuwa Mungu alijua hili, akasema maneno haya:

*"…Umchukue sasa mwanao, mwana wako wa pekee, Isaka..."*

**Sasa Ibrahimu alifanya nini?**

**Wewe ungedhihirisha nini** kama ungekuwa katika nafasi ya Ibrahimu? Je, ungemchukua mtoto wako umbali fulani hadi mlimani...
Na kumtoa awe sadaka ya kuteketezwa kama mungu angekuagiza? **Fumba macho na tafakari jambo hili!** Hili ni halisi! Si hadithi ya kubuniwa! **Ibrahimu alimtii Mungu** na alijitahidi **kutoonesha hofu wala huzuni** usoni alipomwambia Sara kuhusu safari na Isaka!! Huenda alimwambia: "Ninamchukua mtoto nami kwa sababu Mungu amenituma kutoa sadaka mlimani umbali wa siku tatu..." Kisha Ibrahimu **akaandaa kila kitu** na akaanza safari kuelekea **MORIA** — mlima ambao Mungu alimtaja.

Kisha, siku ya tatu ya safari hiyo, alipoiona **mlima wa moria**, aliwaambia watumishi wake wasubiri umbali fulani, na kisha akasema kitu CHA AJABU sana kwao: **Mwanzo 22:5**

*"Ibrahimu akawaambia vijana wake, Kaeni ninyi hapa pamoja na punda; mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kurudi tena kwenu."*

Sasa, je, umeona **imani ya ibrahimu**? Licha ya kujua kwamba Mungu alikuwa amemwagiza amtoe **Isaka awe sadaka ya kuteketezwa**?? **Nini kilimpa imani hii?** Ibrahimu aliwezaje kusema maneno haya, hali alijua kwamba Isaka ndiye aliyepaswa kutolewa dhabihu?

Hakika Ibrahimu **hakuweza kusema uongo kwa watumishi wake!** Sasa hebu **tuingie ndani ya fikra za Ibrahimu** na tuone nini kilikuwa kikipita akilini mwake... Ibrahimu alikuwa ametumia **usiku miwili ya safari** kuelekea Moria bila kupata usingizi mwingi. Ni dhahiri alikaa macho usiku kucha akifikiria kuhusu: **Kusudi la mungu katika kumwagiza amtoe mwanawe mpendwa Isaka kuwa sadaka!**

Je, si Mungu huyo huyo alikuwa amemuahidi miaka michache iliyopita kabla ya kuzaliwa kwa Isaka kuwa **kupitia kwake uzao wa baraka utakuja?** Na je, si **kuzaliwa kwa Isaka** yenyewe kulikuwa **muujiza** wa uwezo wa Mungu — kwa kuwa Sara alikuwa:

- **Amezeeka**,
- **Na yuko katika hali ya kukoma hedhi**, kama tunavyosoma katika:

**Mwanzo 18:11–12** *"Sara alikuwa amekoma kuwa na desturi ya wanawake. Basi Sara akacheka moyoni mwake…"* Na baada ya haya yote, sasa Mungu anamuagiza: **Amuue mtoto huyo huyo**, na amtoe awe: **"sadaka ya kuteketezwa"?**

Ndiyo! Na alipokuwa akitafakari mambo haya na kutazama anga, na kutafakari juu ya "mbingu" na "utukufu wa Mungu", wazo likaanza kuchomoza akilini mwake kwamba Mungu:

**Kwa namna Fulani angemrudisha mtoto wake akiwa hai!** Hakujua **jinsi**, lakini **ALIJUA TU** na... **ALIAMINI!**

Yote haya ndio yalimsababisha kusema maneno ya imani kwa watumishi wake!

Ndiyo! Ibrahimu alikuwa mtu wa kwanza kufikiri kuhusu **ajabu kuu ya...** ***ufufuo kutoka katika wafu!*** Lakini bado jaribio la mwisho la imani ya Ibrahimu **halikuwa limekamilika!** Tunasoma katika: **Mwanzo 22:9–10** "*Wakafika mahali alipoambiwa na Mungu; Ibrahimu akajenga madhabahu pale, akapanga kuni, akamfunga Isaka mwanawe, akamlaza juu ya madhabahu, juu ya kuni. Ibrahimu akanyosha mkono wake, akatwaa kisu ili amchinje mwanawe.*"

Ndiyo! Ibrahimu alikuwa amefika katika kilele cha IMANI yake! Walikuwa wamefika **Mahali Pa Sadaka!!** Walikuwa wamefika mlimani aliotajwa na Mungu – **MLIMA MORIA.** Na walipokuwa wakipanda mlima, Isaka mdogo akauliza swali lile la kuogofya, kama tunavyosoma katika: **Mwanzo 22:7** *"…Akasema, Tazama, moto na kuni; lakini mwanakondoo wa sadaka ya kuteketezwa umo wapi?"* Hakika swali hilo lilipaswa kumletea **kikohozi cha hisia Ibrahimu**; lakini alimjibu kwa **imani** kama tunavyosoma: **Mwanzo 22:8** *"Ibrahimu akasema, Mwanangu, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa...*

Kisha wakafika mahali pa sadaka, na Ibrahimu akajenga madhabahu – na **wakati ukafika wa Ibrahimu kumwambia Isaka**: ***kwamba yeye ndio sadaka hiyo*!!** Unaweza kuwaza Ibrahimu akigeuka, baada ya kukamilisha madhabahu, na kumwita mwanawe akisema: "Isaka, mwanangu, ulikuwa umeuliza kuhusu sadaka, unakumbuka?! Sasa madhabahu iko tayari na inasubiri sadaka. Je, unajua ni sadaka gani Mungu aliyeniagiza nitoe juu ya madhabahu hii?" Isaka anaweza

kujibu: "Baba, si uliniambia kuwa Mungu atajipatia mwanakondoo kwa sadaka? Sioni mwanakondoo! Uko wapi?"

Kisha **Ibrahimu, Akijaa Hisia**, na kwa **sauti ya majonzi yenye ujasiri**, angemjibu: "Mwanangu, mwanakondoo ambaye Mungu amejipatia kwa ajili yake ni **wewe**!"

Ni Mshtuko Gani Huu Ulikuwa Kwa Isaka! Lakini alitambua haraka **IMANI KUU ya baba yake kwa Mungu**, na akachagua **kujitoa mwenyewe pia kwa mapenzi ya Mungu mkuu, mwenye upendo na rehema**, ambaye alikuwa akimwamini na kumwabudu tangu alipokuwa mtoto mdogo! Ndipo mikono na miguu yake ikafungwa, naye akalala juu ya madhabahu ya sadaka!
Na **Ibrahimu akakabiliana na kilele cha jaribu lake!!**

Akatoa **KISU** kutoka kwenye mfuko wake, huenda akakinoa juu ya mwamba, kisha akaweka mkono mmoja juu ya shingo ya Isaka na mkono mwingine akanyanyua kisu juu!!

Kisha katika wakati huo wa mwisho sana, Mungu akaingilia kati kupitia **"malaika wa Bwana"** na akamzuia kama tunavyosoma: **Mwanzo 22:12** *"Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtende neno;..."* Ndiyo! **Ibrahimu akawa – "Baba wa Imani."**

Ni safari ya aina gani hii ilikuwa!Na ni somo la aina gani kwetu ambao tunaahidiwa **thawabu kubwa zaidi kuliko Ibrahimu**!Tafakari ni kwa kiasi gani **IMANI YETU inapaswa kuwa kubwa zaidi!!** Kisha baada ya kusema maneno hayo, Mungu akampa ahadi hii kama tunavyosoma:

**Mwanzo 22:15–18** "*Malaika wa Bwana akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni, akasema, Hakika nitakubariki, na uzao wako nitauzidisha sana kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani ya bahari; na*

*uzao wako utamiliki mlango wa adui zake; na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa; kwa sababu umeyatii sauti yangu.*"

Hii inaitwa...**"AHADI YA IBRAHIMU" (THE ABRAHAMIC PROMISE)** Mungu alimwahidi Ibrahimu kwamba **uzao wake (watoto wake)** ungekuwa: *"kama nyota za mbinguni"* na *"kama mchanga wa pwani ya bahari"!*

**Hii inamaanisha nini?** Inawakilisha **MADARAJA MAWILI** ya watoto wa Ibrahimu ambao kupitia kwao Mungu angemimina baraka kwa: **"jamaa zote za dunia."** Sasa, ni akina nani **madaraja haya mawili ya watoto wa Ibrahimu?**

**Daraja La Kwanza La Uzao Wa Ibrahimu:** *"…kama nyota za mbinguni…"* Je, daraja hili ni nani na linawakilisha akina nani? Kumbuka katika Biblia, neno **"mbinguni"** lina maana ya: **Utawala wa kiroho usioonekana**, kama tunavyosoma katika:

**Mathayo 24:35** "*Mbingu na nchi zitapita...*" Hivyo, uzao huu wa Ibrahimu unawakilisha: **uzao wa kiroho wake!**

Ni akina nani hawa? Tunasoma jibu katika: **Wagalatia 3:7** "*Basi jueni ya kuwa walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu.*" Ndiyo! **Wakristo** ambao ni waaminifu kwa Mungu na **"ni wa imani"** wanakuwa **watoto wa kiroho wa Ibrahimu!** Nao pia wanatajwa kama tunavyosoma katika: **Waebrania 3:6** "*Lakini Kristo, kama Mwana juu ya nyumba yake; nyumba yake ndiyo sisi, ikiwa tutashikamana na ujasiri na fahari ya tumaini hili bila kuyumbayumba mpaka mwisho.*"

Ndiyo! Hivyo basi, **KANISA** au **MWILI WA KRISTO** ndio: **Watoto wa kiroho wa Ibrahimu – "kama nyota za mbinguni." Sasa daraja la pili la uzao wa Ibrahimu:** *"…kama mchanga ulioko pwani ya bahari…"* Daraja hili ni nani na linawakilisha akina nani? Kwa kutumia mfano

huu, linawakilisha: **Watoto wa kibinadamu, wa kimwili wa Ibrahimu.** Hawa ni wale waliokuwa waaminifu kwa Mungu kutoka taifa la Israeli – **wazao wa mwilini wa Ibrahimu!** Wao ndio: **Watoto wa asili wa Ibrahimu.** Nao wanatajwa kama tunavyosoma katika:

**Waebrania 3:5** "*Na Musa kweli alikuwa mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu kama mtumishi, kwa ushuhuda wa mambo yatakayonenwa baadaye;*"Ndiyo! Daraja hili la **watoto wa asili wa Ibrahimu** linajumuisha **Musa**. Hii ilikuwa...

***"Nyumba Ya Watumishi"*** Ambayo ilianza na **Abeli** na kuishia na **Yohana Mbatizaji!** Hivyo basi, ni kupitia Ibrahimu ambapo: **AHADI YA UZAO WA BARAKA** ilitajwa tena: **BAADA YA BUSTANI YA EDENI!** Na ilikuwa ni ahadi ya **kiapo**, kama tunavyosoma waziwazi: *"…Kwa nafsi yangu nimeapa, asema Bwana…"* Mtume Paulo anaeleza **thamani ya ahadi hii ya kiapo** katika: **Waebrania 6:13–18** "*Kwa kuwa Mungu alipomwahidia Ibrahimu, kwa kuwa hakuweza kumwapia mwingine aliye mkuu kuliko yeye, alijiapia mwenyewe, akasema, Hakika kubariki nitakubariki, na kukuongeza nitakuongeza… Mungu, akitaka kwa mwingi zaidi kuwaonyesha warithi wa ahadi kutokugeuka kwa shauri lake, alithibitisha kwa kiapo; ili kwa mambo mawili yasiyoweza kubadilika, ambayo katika hayo haiwezekani Mungu kusema uongo, tupate faraja kuu, sisi tuliokimbilia kushika tumaini lililowekwa mbele yetu.*"

Ndiyo!
Mungu hawezi kufanya mambo **MAWILI tu**:

1. **Hawezi kusema uongo**
2. **Hawezi kuvunja agano.**

Ahadi hii **imehakikishwa na kuhakikishiwa!!** Lakini haikutimizwa **katika maisha ya Ibrahimu** hata kidogo!

**Itatimizwa Lini?**

Ahadi hii **haikutimizwa** wakati wa maisha ya Ibrahimu, lakini **ilirudiwa na kuthibitishwa** kwa vizazi vyake viwili vinavyofuata. Ndiyo! Ilirudiwa kwa mwanawe **Isaka**, na mjukuu wake **Yakobo**, kama tunavyosoma katika: **Mwanzo 26:4 / 28:14** "*Nitazidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na nitawapa uzao wako nchi hizi zote; na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa.*" "*Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea magharibi, mashariki, kaskazini na kusini; na katika wewe na katika uzao wako jamaa zote za dunia watabarikiwa.*" Ah! Uthibitisho wa **"Ahadi ya Ibrahimu"** Hata Baada Ya Kifo Cha Ibrahimu! Kisha mamia ya miaka baadaye, mtunga-zaburi **Daudi** alikumbuka ahadi hii kama tunavyosoma katika: **Zaburi 105:8–11** "*Amekumbuka agano lake milele, neno aliloamuru kwa vizazi elfu moja; agano alilofanya na Ibrahimu, na kiapo chake kwa Isaka; akakithibitisha kwa Yakobo kuwa amri, Na kwa Israeli kuwa agano la milele; akisema, Nitakupa wewe nchi ya Kanaani kuwa fungu la urithi wenu.*" Hivyo basi, **ahadi ya Ibrahimu** ilipitishwa na kuthibitishwa kwa vizazi viwili vilivyofuata! Baada ya Yakobo, **mrithi wa ahadi hiyo alikuwa YUDA**, kama tunavyosoma katika: **Mwanzo 49:9–10** "*Yuda ni mwana wa simba; Ewe mwanangu, umetoka katika mawindo; ameinama, amelala kama simba, na kama simba mzee; ni nani atakayemwamsha? Fimbo ya enzi haitazidi kuondoka kwa Yuda, wala mfanya sheria kutoka kati ya miguu yake, hata atakapokuja Shilo; naye atakuwa ni tumaini la mataifa.*" Ndiyo! Kati ya wana kumi na wawili wa Israeli (Yakobo), aliyebarikiwa alikuwa **Yuda!** Sasa ni nani aliyepaswa kuwa **"uzao wa mwanamke"** aliyezaliwa kutoka ukoo wa Yuda? Tunaona jibu katika:

**Wagalatia 3:16**"*Basi ahadi zilinenwa na Ibrahimu na uzao wake. Haikusema, Na kwa wazao wake, kama kwa wengi; bali kama kwa mmoja, Na kwa uzao wako, ndiye Kristo.*" Ndiyo! **Uzao wa Ibrahimu — "nyota za mbinguni"**, Kama tunavyosoma hapa, alikuwa ni:

**KRISTO!**

Lakini kuna **Fumbo Kuhusu Kristo!** Tunasoma kuhusu hili katika:

**Waefeso 1:22–23** *"…akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake…"* Ndiyo! Hivyo basi tunaona kwamba huu **"uzao wa mwanamke"** — yaani **KRISTO**, **ANA KICHWA…** NA **ANA MWILI PIA!**

Ndiyo! **Yesu ndiye KICHWA**, na **KANISA ni MWILI WAKE.** Na wote wawili ni **warithi pamoja wa "ahadi ya Ibrahimu."** Tunasoma hili kwa uwazi katika: **Wagalatia 3:7, 29** "*Basi jueni ya kuwa wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu.*" "*Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.*"

**Si ni dhaahiri sana?** Sasa hebu tuone zaidi kuhusu **"mwili" wa "uzao wa mwanamke"** kama tunavyosoma katika: **Ufunuo 14:1** "*Kisha nikaona, na tazama, Mwana-Kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na pamoja naye watu mia arobaini na nne elfu, waliokuwa na jina la Baba yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao.*"

Je, umeona hilo? Wale waliokuwa **"pamoja na Mwana-Kondoo"** ndio **MWILI WAKE!** Mwili huu ulioko pamoja naye umeelezwa kuwa na idadi ya **"mia arobaini na nne elfu" (144,000)** Tena, tunasoma kuhusu kundi hili hili katika: **Ufunuo 17:14** "*Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana-Kondoo atawashinda,*

*kwa kuwa ni Bwana wa mabwana, na Mfalme wa wafalme; nao walio pamoja naye ni walioitwa, na wateule, na waaminifu.*"

Ndiyo! Mwili huu hapa tena **uko pamoja naye**, na wanaitwa: **"Waliyoitwa, na wateule, na waaminifu." Hii inamaanisha nini?** Huu ni mchakato wa **KUKUA NA KUKAMILIKA** kwa **"mwili wa Kristo" — yaani KANISA**, kabla ya **kufikia utukufu pamoja na Bwana Yesu!** *(Hili tuliliona kwa undani katika masomo #17, 18, na 19.)*

Hivyo basi, **"uzao wa mwanamke"** ni **KRISTO – YESU akiwa KICHWA**, na **mwili wa 144,000**.

**Je, uchaguzi huu unafanywaje?** Tunasoma kuhusu hili katika: **Yakobo 1:18** "*Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa kwa neno la kweli, tupate kuwa kama limbuko la viumbe wake.*" Ndiyo! Hili linahusu **kuzaliwa kwa njia ya neno la kweli**, ili wawe **limbuko la wokovu wa dunia!** Na Mungu huchagua NA KUTEUA kutoka katika **watu wote wa mataifa yote**, kama tunavyosoma wazi katika: **Ufunuo 5:9** "*Kwa kuwa umewachukua kwa Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila, na lugha, na jamaa, na taifa.*"

Ndiyo! Hawa ndio **limbuko** la 144,000! Lakini hili halifahamiki vizuri na wakristo wengi leo! Kwa nini hivyo? Kwa sababu tunasoma jibu katika: **Warumi 16:25** "*Siri ile iliyofichika tangu milele, sasa imefunuliwa...*"

Ndiyo! Jambo hili ni **SIRI!** Hivyo basi, **"uzao wa mwanamke" — yaani KRISTO** ni siri, na **NJIA** ya kuwa sehemu ya uzao huo imetajwa na Bwana Yesu katika: **Mathayo 7:14** "*Kwa maana mlango ni mwembamba, na njia iendayo uzimani ni nyembamba, nao waionao ni wachache.*"

Ndiyo! Ni njia nyembamba kweli! Ni wachache sana wanaoielewa na kuipata njia hii! Ndiyo, ni "njia nyembamba" sana! Lakini huu ndio

**"uzao"** ambao mwishowe uta: **"kuponda kichwa cha nyoka"** *(Mwanzo 3:15)* kama tunavyosoma katika: **Warumi 16:20** "*Na Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi...*" Ndiyo! Kanisa litakuwa **CHOMBO cha kuangamiza Shetani na nguvu zake za uovu. Hivyo ndivyo utakavyotimia UNABII uliozungumzwa katika bustani ya Edeni maelfu ya miaka iliyopita!** Sasa hebu tuelewe ni nani **"uzao wa nyoka"**, na ni nini **uadui** utakaojitokeza kati ya mizao hii miwili, kama tunavyosoma katika:

**Mwanzo 3:15** "*Nami nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake;*" Tukiwa tumeutambua waziwazi **"uzao wa mwanamke"** kuwa ni:

**KRISTO – KICHWA na MWILI,** Ni nani basi huyu **"uzao wa nyoka"** aliye katika **UADUI na Kristo**? Tunaona kama tunavyosoma katika: **Yohana 8:38** *"…mimi ninenalo nililoliona kwa Baba yangu; nanyi mwatenda hayo mliyoyaona kwa baba yenu."* Haya ni maneno ya Yesu akizungumza na Wayahudi — akisema kuwa **wana Baba mwingine tofauti na Mungu!!**

Tazama jibu la Wayahudi: **Yohana 8:41** "*Sisi hatukuzaliwa kwa uasherati; tuna Baba mmoja, ndiye Mungu...*" Ah! **Wanadai kwamba Mungu ndiye Baba yao!** Lakini Yesu akawahoji kwa hoja kama tunavyosoma katika: **Yohana 8:42–43** "*Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda mimi... Lakini kwa sababu mimi nasema iliyo kweli, hamsadiki.*" Ndiyo! Yesu anawaambia kuwa **Mungu hawezi kuwa Baba yao**, kwa sababu hawampendi wala kumkubali.

Kisha yesu anawataja baba yao wazi kabisa: **Yohana 8:44** "*Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi...*" Ndiyo! **Baba wa uongo!** Wayahudi walikuwa **wamekuwa watoto wa Shetani!**

Hivyo basi... **Wayahudi wenyewe walikuwa "uzao wa nyoka" dhidi ya kichwa cha kristo — yesu!** Walimkataa vikali, na uadui wao

ulifikia kilele kwa: **Kumuua Yesu Msalabani!** Tazama maneno waliyotumia walipodai Yesu asulubiwe, **Mathayo 27:23–25** "*Wakasema zaidi, Na asulibiwe! ... damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu!*" Hivyo basi, kwa **YESU BWANA WETU, KICHWA cha "uzao wa mwanamke"**, **"uzao wa nyoka"** walikuwa ni **Wayahudi**, na **uadui wao dhidi ya Yesu ulikuwa dhahiri** kama tunavyosoma katika andiko hili.

**NA JE KUHUSU MWILI WA KRISTO?**

Tunasoma jibu katika: **Mathayo 13:24–26** "*Akaleta mfano mwingine kwao, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika shamba lake; lakini watu walipokuwa wamelala, adui yake akaja, akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake...*"

**Mfano huu unamaanisha nini?** Tunasoma tafsiri yake kutoka kwa Bwana Yesu mwenyewe katika: **Mathayo 13:38–39** "*Shamba ni ulimwengu; na ile mbegu njema ndio wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu; na yule adui aliyepanda ni Ibilisi...*" Ndiyo! Hii inazungumza kuhusu **MAKUNDI MAWILI YA WAKRISTO** katika **kanisa (shamba)**:

1. **Kundi la kwanza**: watoto wa Mungu
2. **Kundi la pili**: watoto wa Shetani


**Hii ndiyo KWELI!** Yesu MWENYEWE anatuambia jambo hili!

Je, Unajuliza Kivipi? Vema, kama vile Wayahudi walidhani Baba yao ni Mungu lakini walimkataa Yesu, Hivyo hivyo, **wakristo hawa** watajidai kuwa wa Kristo lakini **watapinga Wakristo wa kweli na kweli wanayoisimamia.** Na hivyo ndivyo **uadui utakavyokuwapo kati ya na ndani ya Wakristo wenyewe** — kati ya wale **kwa jina tu** na wale **wa kweli!**

**JE, UMESTAAJABU?**

Naam, tutajifunza hili kwa undani zaidi katika somo lijalo kuhusu **"uadui"** na **mwisho wake**, kama tunavyosoma: *"...atakupiga kichwa, nawe utampiga kisigino."* Ndiyo! Andiko hili la UNABII limo karibu **KUTIMIA KATIKA SIKU ZA KARIBUNI**, na ninyi wapendwa ndugu na dada: **mtaona na bwana akipenda, mtakuwa sehemu yake!**

**AMINA….**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***